# SURA YA SABA

**Baraka Za Kifedha**

Mungu anapenda kuwashugulikia watu wake! Hatuhitajiki kamwe kuomba tukidhiwe kwa sababu Mungu anaweza na hutaka kutoa kwa utele kwa ajili yetu.
"*Nilikuwa kijana nami sasa ni mzee, lakini sijamwona mwenye haki amaechwa wala mzao wake akiomba chakula"* (Zaburi 37:25)
Tunapomtafuta Bwana, hatutakosa yaliyo mema. Sababu? Mungu ndiye mpaji.
"*Mcheni Bwana enyi watakatifu wake, yaani wamchao hawatahitaji kitu chochote kilicho chema*"(Zaburi 34:9-10)
Kila siku namshukuru Mungu kwa sababu ya ukarimu wake. Pia najua mwafanya hivyo. Unafikiria ulipata kazi yako jinsi gani? Unakipataje chakula chako?
Ulienda kazini, ukatoa jasho… lakini nani alikupa hiyo kazi? Tunapomtafuta Mungu atatukarimia.

**Ukarimu wa Mungu ulio mzuri.**

"Mwanangu usisahau sheria yangu, bali moyo wako uzishike amri zangu. Maana zitakuongezea wingi wa siku. Na miaka ya uzima, na amani (ufanisi)" (Tunza: ufanisi unatokana na kuzitii sheria za Mungu au neno lake katika nyoyo zetu.)

*"Rehema na ukweli zisifarakane nawe; zifunge shingoni mwako; ziandike juu ya kibao cha moyo wako.ndivyo utakavyopata kibali na akili nzuri, mbele ya Mungu na mwanadamu. Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako. Usiwe mwenye hekima machoni pako, Mche Bwana, ukajiepushe na uovu. Itakuwa afya kitovuni pako na mafuta mifupani mwako.*
*Mheshimu Bwana kwa mali*(utajiri*) yako, na kwa malimbuko*(Zaka) *ya mazao yako yote. Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi, na mashinikizo yako yatafurika divai mpya*.' (Mithali 3:1-10)
Hizi ni faida tuzipatazo kutoka kwa Mungu na ukarimu wake kwetu tunaolitenda neno lake. Tunapoheshimu Mungu kwanza kwa kile alichotupatia, tukimkiri katika njia zetu zote yeye atakarimia kwa ajili yetu.
Tusitegemee hekima na ujuzi wetu. Tutumaini Mungu atushughulikie tunapomtambua au kumkiri kama chanzo cha maelekezo, atayanyosha mapito (njia) yetu na kutufanikisha. (Zaburi 1:2-3, Yoshua 1:8) hatupaswi kuyasukuma mambo yatendeke tunapomsifu na kumshukuru Mungu tunapotenda kulingana na neno lake. Mungu ataifungua milango. Tunapoenenda kwa utiifu katika neno lake na kushuhudia ulimwengu kuwa Mungu ni mapaji, Mungu naye atatukimia.

Ni muhimu kuyafanya mambo yetu katika utauwa kwa unyofu na kweli. Tunapotafuta kuhifadhi mtazamo kuwa chochote tukifanyacho, tunakifanya kwa utukufu wa Mungu, basi Mungu naye atatukimu.

**Miujiza ya ukarimu wa Mungu katika Biblia**

Nasisimuka ninapoitazama miujiza ya ukarimu wa Mungu ikidhihirika katika neno lake. Mungu alimkarimia Eliya, nabii wa Mungu wakati wa ukame kwa kuwatuma kunguru wamlishe. Mungu aliwatuma kunguru kama wajumbe wa ukarimu wake (1 Wafalme 17:4-7)

Katika hesabu nyingine, Eliya alimjia mjane aliyekuwa akioka mikate kwa ajili yake na mwanawe. Wangekufa kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Wakati Eliya alisema, "Niletee nakuomba, kipande cha mkate mkononi mwako," hakumwazia kifo mjane huyu kwa sababu ya njaa. Alichokisema ni: toa unipatie naye Mungu atakushughulikia!" Wakati yule mjane alienenda kwa imani na kutoa alichokuwa nacho kumpa mtu wa Mungu, ukarimu wa Mungu ulimjia. Hakukosa chakula wakati wa kipindi chote cha ukame kwa sababu Mungu alikuwa akijaza lile pipa la unga na chupa ya mafuta. Huu ulikuwa muujiza wa Mungu wa ukarimu wake.

Naamini kuwa hata leo Mungu ni wa miujiza. Yeyote amwitaye hatakosa yoyote yaliyo mema. Anataka kuwakarimia wale ambao kwa upendo wametazamisha nyoyo zao na akili zao kwa Mungu.

Kitabu cha Hesabu kinaonyesha jinsi Mungu alivyowapa Wanaisraeli manna asubuhi na jioni nyama. Alimfanya Musa kulipiga jiwe ili wapate maji. Huu pia ulikuwa muujiza wa ukarimu wa Mungu. Fahamu kuwa watu hawa walikuwa wakizunguka zunguka sehemu iliyokuwa jangwa ya Sinai. Jangwani Mungu aliwakimu kwa miaka arobaini. Manna (mkate) asubuhi na nyama jioni, maji na viatu vyao havikuchakaa (Tazama Kumbukumbu la Torati 8) walipomtegemea Mungu awakimu kikamilifu. Huyu ndiye Mungu ninayemjua na kumwamini. Huyu ndiye pia anayetaka kukupenda na kukushughulikia. Anataka kuenenda kulingana na neno lake kwa ajili ya watu wake wanaomwamini kulingana na neno lake na kulitenda. Usinielewe vibaya sisemi uiache kazi yako ili Mungu akushughulikie. Kazi yako ni sehemu ya ukarimu wa Mungu. Ninalolisema ni kuwa, tunapoenenda katika utiifu, na tusiwe wavivu, lakini tukimwamini Mungu kama chanzo cha upaji, sio kazi zetu, atatukimia. Hatutakosa yaliyo mema kamwe.

Yesu alipokuwa hapa aliwalisha zaidi ya watu elfu tano kwa samaki wachache na mikate michache; na kulikuwa na mabaki tele. (Yohana 6:1-13). Nakuhimiza leo umtazame, "*Mungu awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu"* (Waefeso 3:20) Mungu anaweza kutukimia vyema kutushinda sisi sehemu zote za maisha yetu- kiroho, kiakili na kimwili, kifedha na mahusiano.

Tukianza kumtazama Mungu kama mpaji wetu na kufahamu kuwa ukarimu wake wapita chochote tuwezacho kukifikiria, basi hatutakumbwa tena na hofu au woga.

Ukombozi pamoja na uponyaji ni mambo yaliyotendeka katika huduma ya Yesu na hutendeka hata leo. Tutaiona miujiza mingi tunapomtarajia Mungu kufanya zaidi. Tunaishi katika siku za miujiza. Yesu anarudi. Miujiza inatendeka kwa wale wamtazamao Mungu, wakiamini kuwa atafanya alisemalo na kutenda kulingana na neno lake wakimwamini na kumtumainia. Wanaamini kuwa Mungu anaweza kuwapa chochote wanachokihitaji katika maisha yao. Mungu anaweza na anataka kuponya. Anaweza na kutaka kubariki ndoa. Anaweza na kutaka kufanya yasiowezekana kwa niaba wale waaminio. (Mariko 9:23)

Wanafunzi walipotumwa na Yesu waliagizwa wachukue kanzu moja (si kabati nzima) na wasichukue mkoba wala viatu. (Mathayo 10:9-10)Naamini kuwa Yesu alitaka kuwatuma hivyo ili awadhihirishie kuwa walitakiwa kumtazama Mungu pekee kutosheleza mahitaji yao. Waliporudi, Yesu aliwauliza, *"Je! Hapo nilipomtuma, mlipungukiwa kitu?"walimjibu kwa furaha, "La! Hatukupungukiwa*!"(Luka 22:35) walimtegemea Mungu. Hawakutakiwa kuwa na kabati iliyojaa mavazi, jokofu lililojaa chakula au akaunti nono katika benki. Mungu angewapa kila kitu walichohitaji.

Sio vibaya kuwa na kabati lililojaa mavazi mazuri, jokofu linalojaa vyakula au akaunti nono katika benki. Hata hivyo tunatakiwa kumtegemea Mungu atutimize mahitaji yetu. Hatutakiwi kujitegemea au kutegemea mapato yetu yakiwa madogo au makubwa. Tumtarajie Mungu ayatimize mahitaji yetu.

Wanaisraeli walipokuwa wakijiwekea manna, yalikuwa yakiharibika keshoye. Mungu alikuwa akiwafunza kumtegemea na kumtumainia siku hadi nyingine. Tazama Kumbukumbu la Torati. Hakuna siku alikosa kuwatimizia mahitaji yao. Tuna Mungu aliye mwaminifu na wa ajabu.

**Aina zingine za ukarimu**

Wokovu wetu unategemea ukarimu wa Mungu kwa kuwa uzima wa milele unakarimiwa na Mungu pekee. Hatungeupata wala kuufanyia kazi. Hatungekuwa na uzima wa milele ikiwa Mungu hangeutoa kwetu. Kupitia upendo wake alitukarimia uzima huu kupitia kwa Yesu Kristo. Tunapaswa kuupokea ukarimu wake kwa kumkiri Bwana na kuokolewa (Warumi 10:9-10)

Mungu ndiye hufanya mvua kunyesha na mimea kukua. Mungu ndiye hutupatia uwezo tulionao na kazi tunazofurahia yeye ndiye husababisha mema yote katika maisha yetu. Tunapomuenzi Mungu yeye atatembea bila pingamizi yoyote kwa ajili yetu. (Mithali 3:5-6)

Haya yote yanaweza kuonekana ujinga mbele ya watu wa dunia ambao hutaka kujiwekea na kuhodhi mali wakifikiria, "Nikikosa kuyaweka mali ninapoyapata itatokea kuwa sitakuwa nayo." Kwa hivyo hujiwekea gesi, kusitokee uhaba wa gesi, chakula kusiweze kutokea uhaba wa chakula n.k. "Nilicho nacho lazima nijiwekee," dunia husema.

Uupatapo ukarimu wa Mungu, usisahau kuwa ndiye akupaye. Usifikiri yeyote unayemjua ndiye alikupa ama uwezo wako mkuu wa kiakili bali ni Mungu. Jua kuwa Mungu ndiye mpaji wako. Anasema, "Usinisahau wakati mema yanatendeka kwako." Shukuru kwa kile ulicho nacho, kiwe kidogo au kikubwa. Mshukuru kwa ukarimu wake na ukatae kunung'unika na kutoridhika. Unapomfurahia Mungu na neno lake nazo ahadi zake zitaanza kutimizika kwako. Utaanza kuelewa, "Ndio, Mungu ana lingine zuri kwangu. Unapolitenda neno la Mungu, Mungu anaanza kufanya lile alisemalo usisahau anakupenda na anasabibisha baraka kwako..

Kijana mmoja katika mmoja wa mikutano yetu aliamua kutoa fungu la kumi kutoka kwa jumla ya mapato yake kwa kazi ya Mungu kwa mara yake ya kwanza. Wiki iliyofuata Bwana alimpatia makazi ambayo hangeyapata awali, akapata cheo kazini na gari. Mungu alitimiza neno lake wakati yule kijana alitoa kwa upendo kutoka kwa moyo mtiifu.

Kila kitu kilimwendea vizuri kijana yule, jinsi Mungu alivyoahidi. (Kumbukumbu la Torati 8:6-20, Malachi 3:8-12) Hata hivyo alianza kufikiria kuwa ndiye alisababisha yale yaliyotendeka. Aliamini uongo wa Shetani. Tulisikia kuwa aliyarudia mambo ya dunia. Hakumtamani tena Mungu nayo ile kazi aliyoipenda iligeuka kuwa chukizo. Alikuwa amesahau ni nani chanzo cha uhai wake na ukarimu. Nashiriki nawe jambo hili kama ukumbusho, "*Kwa hivyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke*!" (1 Wakorintho 10:12)

Mungu anakupenda na anataka kukukarimia, unapoendelea kulitii neno lake, baraka za Mungu zitaendelea.

**Mwanadamu anavyopokea ukarimu wa Mungu.**

Katika Mathayo 6:31-34 Bwana Yesu anatuambia tusisumbuke basi mkisema, tule nini? Au tunywe nini? Au tuvae nini?  n.k kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta. Ikiwa mioyo yetu inawangazia Mungu, tukiwa na Yesu kama Bwana, Mungu tayari ametukarimia kutoka ghala lake.

Mungu anatuelekeza vile tunavyoweza kupokea kutoka ghalani mwake. *"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake"* (Mathayo 6:33) Yeye atatutimizia mahitaji yetu anayoyajua vyema kutushinda. Tusisumbuke, sehemu yetu ni kumtafuta Mungu, nayo sehemu yake ni kututunza. Kusumbuka kwetu kutazuia ukarimu wake kutujia. Tunapaswa kumshukuru na kumsifu Mungu kwa utele wa ukarimu wake kwetu.

*Ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni na ndege wa angani, je! Hatazidi sana kutuvisha utukufu wa uumbaji wake?* (Mathayo 6:30) "*Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Yesu*" (Wafilipi 4:19)

Mungu tayari ametutimizia mahitaji yetu na anayajua kabla sisi kuomba. (Mathayo 6:8). Anayajua mahitaji yetu vyema kuliko sisi na anataka kututimizia katika utele wake. (Waefeso 3:20)Nii kwa sababu ya utele wa ukarimu wake kwetu ndivyo tunaweza kuwa na ukarimu na furaha kuwatimizia wengine mahitaji yao.

Tunapaswa kuridhika na ukarimu wa Mungu na kukiri kwa vinywa vyetu, *"Sitapungukiwa na kitu"* (Zaburi 23:1)  Ungewazia, "Lakini sina kila kitu ninachohitaji" Fahamu kuwa moyo wako ukimwangazia Mungu na kumshukuru kuwa unakila kitu unachohitaji (chakula, mavazi, usafiri, kazi n.k ) atakukarimia. Mtumainie na usizungumze kamwe kuhusu kukosa na kuhitaji.

Ahadi za Bwana hazitokei tu bure. Mungu husema, "Fanya hivi nami nitatenda." Tunatakiwa kuelewa kuwa Mungu hutwambia tuyatende mambo fulani ili tuweze kuupokea ukarimu wake. Asili ya Mungu ni ukarimu na kutoa kwa utele. Yeye si bahili. Kwa kuwa yumo moyoni mwetu, tunatakiwa kutamani kutoa kwa utele kwa wengine kutokana na kukarimiwa kwetu na Mungu.

**Kuhusu fungu la kumi**

*Tuliangalie fungu la kumi: Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini nyinyi mnaniibia mimi. Lakini nyinyi mwasema, tumekuibia kwa namna gain? Mmeniibia zaka na dhabihu. Nyinyi*

*mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkinijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote yatawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana asema Bwana wa majeshi* (Malaki 3:8-12)

Hili ni neno la Mungu na ahadi kwetu. Waaminio wengi wanazuia ukarimu wa Mungu katika maisha yao. Wao ni walafi na wachoyo kwa ukarimu wa Mungu, wakijihodhia mali wao wenyewe na kutoa masao katika huduma za Mungu badala ya malimbuko ya kwanza kama atarajiavyo. Mungu anawaita "wanaomwibia" ikiwa tunamwibia Mungu  tunatarajiaje atubariki kwa ukarimu wake?

Ni moyo uliojaa shukurani tu unaoweza kukarimia kama Mungu afanyavyo. Ikiwa moyo wako unaangazia tu vitu vya ulimwengu, kupokea baraka baada ya nyingine, basi utakosa baadhi ya baraka kubwa sana za Mungu katika maisha yako. Kutoa ndiyo njia ambayo baraka hutujia. Yesu alisema, "*Ni heri kutoa kuliko kupokea*" (Matendo ya Mitume 20:35)

(Hatumwombi kutoa katika huduma hii. Huduma ambayo Mungu ametupatia inatazamia kulitoa neno la Mungu bure. Atatutunza kupitia wale watu ameongoza kutoa kwetu. Tunataka mfahamu hili neno linalohusiana na ukarimu wa Mungu ndipo muweze kuingia katika ukamilifu wa ukarimu wa  Mungu alio nao kwenu ili muweze kutoa katika huduma zake.)

Mungu katika Malaki 3:8 asema wewe nami twamwiibia ikiwa hatulitoi fungu la kumi la mapato yetu kama shukurani kwake. Mungu anataka kutubariki. Tulifanyalo analolisema, ameahidi kuyafungua madirisha ya mbunguni na kutumwagia baraka zake. Zinatujia kwa njia nyingi tofauti. Hutukarimia siha, huongeza mali na hujumuisha kile tulicho nacho.

Tumegundua baadhi ya watu kanisani wana mali mara mbili au tatu zaidi kutushinda kwa sababu ya ukarimu wa Mungu, lakini sisi tunatoa zaidi kama Mungu anavyotuongoza. (Kuna mengi mema yanayotuzingira yamkini Mungu hataki tuyatolee. Toa pale Mungu amekuongoza baada ya kuomba.)

Mungu atamkemea alaye (Shetani) na hataweza kuiba asilimia tisini kutoka kwetu. Hili litafanyika tunapofanya alisemalo Mungu kwa moyo mkunjufu, wenye utiifu tukikiri ahadi zake na kumwamuru Shetani aiondoe mikono yake kwa kile kilicho  chako. "*Mheshimu Bwana kwa mali yako na kwa malimbuko ya mazao yako yote. Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi na mashinikizo yako yatafurika divai mpya*." (Mithali 3:9-10)

Mungu anataka tutoe kwake kwa hivyo yu huru kutupa. Hahitaji sisi tumpatie. Yeye ametupatia kila kitu tulicho nacho anachokisema ni, (Nipatie moyo wako! Nisifu!" kimsingi, fungu la kumi ni dhabihu ya shukurani kwa Mungu kwa ajili ya yale yote aliyokutendea. Anataka kuona kama mioyo yetu inamwangazia kama chanzo cha ukarimu au tunauangazia ulimwengu.

**Kutoa na Kupokea**

"*Amhurumiaye masikini humkopesha Bwana; naye atamlipa kwa tendo lake njema."* (Mithali 19:17)Tukiwapa maskini tunamkopesha Bwana naye atatulipa kwa matendo yetu mema. Hatutoi tukisema, "Sawa, Bwana, ninatoa kama usemavyo nibariki sasa!" Ukweli ni kuwa atatubariki, hata hivyo usijiingize katika mawazo ya "Nibariki" tunatoa kwa sababu tunamshukuru Mungu kwa ukarimu wake na pia kutupa nafasi ya kuwasaidia ndugu zetu wakati wa uhitaji. Hatutoi kwa maskini tukitarajia makubwa kutoka kwa Mungu. Makubwa yatatujia ikiwa mioyo yetu ni minyofu. Tunawapa maskini kwa sababu tunampenda Mungu. Nakuchochea leo uwape wengine sababu unawapenda na unataka wabarikiwe na Bwana pia. "*Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho (mtoapo) ndicho mtakachopimiwa*" (Luka 6:38)

Mfano huu huonyesha kuwa tukipima mtu gunia kubwa la nafaka, Mungu angetupatia gunia la nafaka ambalo limejaa, limeshindiliwa limesukwa sukwa. Mungu atakupa gunia la uzani wa pauni kumi na tano kwa lile la uzani wa pauni tano ulilotoa.
Huu ni ukarimu wa Mungu.

Kwa nini Mungu afanye hivi? Sio kwamba uweze kuhodhi na kujipatia chochote ulichotaka kupata. Sababu ni uweze kupata kwa wingi ili uweze kutoa. Hii ni njia moja ya Mungu kuwatunza watu wake, anaweza kufanya hivi kupitia kwetu kwa sababu sisi tu watoto wake. Tuna asili ya Mungu- upendo, ukarimu, kusameheana. Tunataka watu wabarikiwe.

Pale ambapo watu wanafanya Mungu alisemalo kwa moyo wenye shukurani pasipo kujitafutia zawadi na sifa, ila wakitafuta kumtukuza Mungu, watu hao hawakosi chochote. Wao wametunzwa vizuri na wanaweza kutoa kila wakati. Hii ni asili ya Mungu- kutoa. Hii ni asili yetu kama watoto wake- kutoa.
Mungu na watu wake ni wakarimu.

Anashughulikia watu wake na huduma zake kupitia kwa watu wanaofahamu kuwa kila kitu tunachokimiliki kimetoka kwa Mungu. Sisi ni watunzaji wa ukarimu wa Mungu; kuutumia kama anavyotuelekeza. Soma Wakorintho 9:6-15.

Tunapotoa kuwapa maskini, wanaohitaji au sadaka ya kipekee (sio fungu la kumi), tunaweza kuamua kile tutakachokitoa au tusitoe. Hatatutakiwi kutoa kwa sababu tumeuona mfuko wa sadaka ukipitishwa. Tuna uhuru wa kuchagua kile tutakachokitoa. Toa kile umejiamulia katika roho yako . Toa kwa ukunjufu ukiiona kama fursa ya kipekee uliopewa. Tunatoa kwa sababu tunampenda Mungu na tunapenda kuwabariki wake kwa huduma na kwa sababu Mungu ametubariki. Tazama 2 Wakorintho 9:6-15 mstari wa 8 na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema kama ilivyoandikwa, ametapanya, amewapa maskini, haki yake yakaa milele.

Mstari 9-10 tunapotoa kwa ukunjufu wa mioyo yetu Mungu atakutana na mahitaji ya watu wake. Atatupatia mbegu zaidi tupande (Neno, mali n.k) ili watu wake wabarikiwe.

Mstari 11 "Mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote umpatiao Mungu shukurani kwa kazi yetu. Mungu anatuambia tutoe kwa ukarimu ili baraka zake zitumwagikie. Hataki tuwe bahili.
Mungu ni mkarimu. Anataka watu wabarikiwe.

Hebu firkiria, je, kuna yeyote karibu nawe sasa anayehitaji kitu unachoweza kumpatia. Mungu anataka ukutanae na hitaji hilo. Lithibithishe neno la Mungu ndani yako kwa kutoa sababu unampenda Mungu na mtu huyo pia.

Mstari 12-14 Maana utumishi wa huduma hii (kutoa) hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukurani nyingi apewazo Mungu; kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo(kutoa) wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kukiri injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote. Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaone shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu.

Sisi hutaka kuwa mashahidi wazuri wa Yesu. Kutoa kwetu ni njia nyingine ya kuwanyoshea wengine uzuri na upendo wa Mungu. Soma Yakobo 2:14-16

Ni tendo lisilo la kiungu tunapowaona ndugu zetu katika uhitaji fulani na kuwaambia "Nitakuombea," au kuwaambia "Mungu atakubariki" na kuwaaga bila msaada wowote. Ni vyema kushughulikia mahitaji yao na kuwaombea. Kuna haja gani kuwaona wengine katika uhitaji na kukosa kuwakarimia? Kutoa kwetu kunaonyesha tuna imani katika Mungu. Tunaweza kutoa vyote tulivyo navyo kama Mungu anavyotueleza na tusikose chochote. Hatuwaambii mtoe mali yenu yote bali tunawaambia kuwa Mungu atakutana na mahitaji yetu yote. Tunapotoa kushughulikia hitaji la mwingine, tunahakika kuwa Mungu atatutunza.

Soma 1 Yohana 3:17-18. Je, upendo wa Mungu unawezaje kuwa ndani mwetu tunapomwona mwenye uhitaji na kukosa kumshughulika. Kwa sababu ya kumpenda Mungu, tunawapa wenye mahitaji. Ni hakika kwamba kadri unavyoendelea kusoma haya, unafikiria huduma na watu ambao unaweza kutolea. Kwa nini? sababu unampenda Mungu na watu wake. Unajali.

Soma 1 Timotheo 6:17-19. Kifungu hiki kinazungumzia matajiri wenye utele wa mali. Tusiutumainie utajiri uishao lakini tutumainie Mungu. Tunatakiwa kuwa wakarimu, tukifanya mema na tukishiriki tulicho nacho na wengine. Tunapofanya hivi hatutaanguka kwenye mtego wa Shetani wa "undanganyifu wa mali" (Mariko 4:19) ambapo roho zetu zinaangazia kutafuta kuhodhi mali ya ulimwengu huu kuliko Mungu. Tumaini letu ni kupata pumziko ndani yake wala sio kiwango cha kilichoko kwenye benki. Kila kitu kilicho cha ulimwengu huu kitapita. Neno la Mungu pekee na imani yetu ndani ya Yesu Kristo aliye chemichemi ya uzima wetu itabaki.

Sio kiwango cha kutoa kwetu kitaleta tofauti. Wengi hufikiri kuwa wakitoa kiwango kikubwa watapata baraka kubwa kweli; hata hivyo Mungu huuangalia moyo wa mtoaji sio kiwango alichokitoa. Nataka uelewe kuwa njia ya pekee ya kutoa ni ya upendo na shukrani kwa Mungu. Yule mjane aliyetoa senti mbili Yesu alisema kuwa alitoa zaidi ya wale wote walitia sadakani katika mali iliyowazidi. Alitoa vyote alivyokuwa navyo kwa Bwana wake. Wale wengine

walikuwa wakitoa sehemu ndogo tu ya kile walichokuwa nacho. Kwa mfano kutoa dola mia tatu ni jambo ndogo sana kwa mtu mwenye mamilioni ya pesa lakini mtu mwingine kutoa dola mia tatu hakika ni sadaka ya upendo.

Wamkumbuka mjane aliyejiwa na Eliya? Alimwomba ampatie mkate wa mwisho aliojitayarishia yeye na mwanawe kabla wafe njaa. Alipotoa ule mkate wa mwisho kutokana na ukarimu wa moyo wake kwa Eliya, Mungu alimtembelea kwa muujiza wa kushughulikia mahitaji ya mwezi baada ya mwingine. Ile chupa ya mafuta na kibaba cha unga kilijazwa na Mungu kwa ukarimu wake.

Fikiria juu ya mjane huyu wakati unapoanza kusema, “Siwezi kutoa, nina kidogo tu kilichobaki.” Nakuchochea uweze kumruhusu Mungu afanye muujiza katika maisha yako. Uweze kuuona ukarimu wa Mungu ambapo unaweza kutoa hata ingawa huna cha kutoa. “Nitatoa nini?” Jitoe wewe mwenyewe. Toa wakati wako, toa mali yako. Mungu ataheshimu kutoa kwako ikiwa unamtolea Bwana, kuwapenda watu wake.

Je, Mungu anawapenda watu wake jinsi gani siku ya leo? Anawapenda kupitia kwa wengine. Sisi tu watoto wake. Mungu ametupatia uwezo wa kuwapenda wengine kwa sababu alitupenda kwanza. Inachukua hatua ya imani kutoa, sio kwa faida au kupata tena bali kwa sababu tunataka wana wa Mungu wabarikiwe. Ili waweze kusema, “Mungu ni mkuu na anastahili sifa, ukarimu wake ni mkuu.” Ikiwa watu hawamjui Yesu watasema, “Kuna jambo lililo tofauti kuhusu hao watu. Wanashughulikia na kutoa ingawa hawana mali nyingi ya kutoa”. Watu wa ulimwengu wanaona tofauti hii kwa sababu njia ya ulimwengu ni kutafuta mali na kuhodhi na kutafuta tena. Njia ya Mungu ni kutoa na kuelewa kuwa Mungu ndiye hukidhi mahitaji yetu yote.

Wengi watampokea Bwana kwa sababu ya ukarimu wetu. Watu hawa watamwona Mungu kupitia sisi. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. (Yohana 3:16-18)

© 2006, Glory To God Ministries International™, all rights reserved
www.glorytogod.org